JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA

SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA

ISO 9001:2015 Certified

*Mwanachama wa Shirika la Viwango la Kimataifa (ISO), Codex Alimentarius Commission (WHO/FAO) na Wakala wa ISO na Mashirika ya Viwango ya Mataifa mbalimbali*

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU USALAMA WA CHAKULA CHA MSAADA KUTOKA MAREKANI ULIOTOLEWA KWA BAADHI YA SHULE ZA MKOA WA DODOMA

**Dar es Salaam, 17 Machi, 2024**

Hivi karibuni, kumekuwepo na taarifa iliyosambaa kwenye mitandao ya kijamii kuhusiana na msaada wa chakula (mchele ulioongezwa virutubishi, mafuta ya kupikia ya alizeti yaliyoongezwa virutubishi na maharage), ambao ulitolewa na Wizara ya Kilimo ya Marekani kwa ushirikiano na Taasisi ya Jumuiya za Kimataifa (Global communities) katika baadhi ya shule za mkoa wa Dodoma chini ya mpango uitwao "Pamoja Tuwalishe".

TBS inapenda kuujulisha umma kuwa chakula hicho kilifuata taratibu za uiungizwaji wa chakula nchini ambapo kilipofika kilifanyiwa ukaguzi na uchunguzi wa kimaabara na kuthibitishwa kuwa ni salama kwa matumizi. Aidha, utaratibu wa kuongeza virutubishi kwenye chakula (food fortification) unakubalika kitaalamu na hufanyika kwa lengo la kuboresha hali ya lishe kwa walaji.

TBS itaendelea kusimamia kikamilifu jukumu la kuhakikisha kuwa chakula kinachoingia nchini kinakidhi vigezo vya usalama na ubora kwa mujibu wa matakwa ya viwango ili kuendelea kulinda afya za walaji.

TBS inawashukuru wananchi wote ambao wanaendelea kutoa ushirikiano kwani suala la udhibiti wa usalama na ubora wa bidhaa ni mtambuka (shared responsibility).

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia kituo cha huduma kwa wateja kwa namba **0800110827.**

Imetolewa na:

**Gladness H. Kaseka**
**<u>MENEJA UHUSIANO NA MASOKO</u>**


**TBS MAKAO MAKUU**
Shirika la Viwango Tanzania
Barabara ya Sam Nujoma / Morogoro, Ubungo, Dar es Salaam
S. L. P. 9524
DAR ES SALAAM, TANZANIA
Simu Na: +255 22 245 0298/ +255 22 245 0206
Nukushi: +255 22 2450959
Namba ya Simu Bila Malipo: 0800110827
Barua pepe: info@tbs.go.tz
Tovuti: http://www.tbs.go.tz
Barua pepe kwa ajili ya malalamiko ya wateja: malalamiko@tbs.go.tz
Twitter: TBS_Tanzania
Instagram: tbs_Viwango

**TBS KANDA YA KATI**
Jengo la Kambarage
S. L. P. 2956
DODOMA, TANZANIA
Simu Na: +255 26 2520310

**TBS KANDA YA ZIWA**
Jengo la NSSF, Ghorofa ya 3
S. L. P. 1814
MWANZA, TANZANIA
Simu Na: +255 28 2505044

**TBS KANDA YA KASKAZINI**
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 2399
ARUSHA, TANZANIA
Simu Na: +255 27 2520143

**TBS KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI**
Jengo la NHIF, Ghorofa ya 7
S. L. P. 1674
MBEYA, TANZANIA
Simu Na: +255 25 2502848

**TBS KANDA YA KUSINI**
Jengo la MTUWASA
S. L. P. 1396
MTWARA, TANZANIA
Simu Na: +255 23 2334477

**TBS KANDA YA MAGHARIBI**
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 1276
KIGOMA, TANZANIA
Simu Na: +255 28 2804023